

Mnamo mwezi November 2013 TASAF awamu ya tatu ilianza kutekelezwa kwa kuainisha kaya maskini sana, jumla ya kaya 1,321 zilitambuliwa na tayari zimeanza kunufaika na Mpango wa kunusuru Kaya Maskini (PSSN). TASAF III itatekelezwa kwa miaka kumi katika Awamu mbili za miaka mitano kila Awamu kaya. Mpango wa TASAF III una sehemu kuu nne za utekelezaji, ambazo ni :-

- Mpango wa kunusuru kaya maskini, ambao unatoa ruzuku kwa kaya maskini sana hususan zenye wajawazito na watoto ili ziweze kupata huduma za elimu na afya. Pia kutoa ajira kwa kaya maskini zenye watu wenye uwezo wa kufanya kazi wakati wa majanga mbalimbali kwa mfano ukame, mafuriko n.k.
- Kuongeza kipato kwa kaya maskini kupitia uwekaji akiba na shughuli za kiuchumi ili kuboresha maisha.
- Kujenga na kuboresha miundo mbinu inayolenga sekta za elimu, afya na maji.
- Kujenga uwezo katika ngazi zote za utekelezaji, sehemu hii endelevu katika kila hatua ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini.

1.1 LENGU kuu la TASAF III ni kuziwezesha kaya maskini sana kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kujiletea maendeleo na kuongeza matumizi muhimu kaya.

1.2 MADHUMUNI YA MPANGO (TASAF III)

- Kuzeweshezesha kaya Maskini sana kuongeza matumizi muhimu kwa njia endelevu.
- kuzewesha kaya maskini kuwa matumizi hasa wakati Hari
- kuwekeza kwenye rasilimali watu hususana watoto.
- kuimarisha shughuli za kuongeza kipato kwa kaya
- kuongeza matumizi ya hudumu za Jamii

1.3 VIGEZO VINAVYOTUMIKA KUTAMBUA KAYA MASKINI SANA

1. Ina kipato cha chini sana na si cha uhakika ukilinganisha na kaya zingine kijijini/mtaa/shehia.
2. Haiwezi kumudu au haina uhakika wa kupata milo mitatu kwa siku; Hii ina maana kwamba kaya ya namna hii haiwezi kupata milo mitatu kwa siku, kifungua kinywa (mlo wa asubuhi), mlo wa mchana na wa jioni kwa uhakika
3. Inaishi kwenye makazi duni sana; Kaya hii inaishi katika makazi duni kupindukia kiasi cha kuhatarisha maisha na afya za wanakaya husika.

4. Kaya yenye watoto wenye umri wa kuwa shule lakini hawajaandikishwa au wameacha shule kwa kushindwa kumudu gharama; Ina watoto ambao hawaendi kliniki kupata huduma za Afya.
5. Kaya haiwezi kumudu kugharamia mahitaji muhimu ya kumwezesha kumpeleka mtoto kliniki kama vile mavazi ya mama na mtoto au bima ya afya
6. Ina watoto wengi, Kaya yenye watoto wengi ambayo haiwezi kumudu kugharamia mahitaji muhimu katika kaya kama vile makazi, malazi, mavazi, chakula, elimu na afya

2.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI KUPITIA TASAFU AWAMU YA TATU(TASAF III) .

MALIPO KWA KAYA MASKINI HADI APRIL 2017.

| MWEZI WA MALIPO | KIASI CHA FEDHA | FEDHA YA WALENGWA | 1.5% YA MTAA | 1% YA KATA | 5% YA LGA |
|------------------------|------------------------|--------------------------|---------------------|-------------------|------------------|
| MAR-APRIL 2014 | 39,034,125.00 | 34,697,000.00 | 591,426.14 | 394,284.09 | 3,351,414.77 |
| MAY-JUNE 2014 | 38,077,875.00 | 33,847,000.00 | 576,937.50 | 384,625.00 | 3,269,312.50 |
| JULY-AUG 2014 | 34,568,626.00 | 30,807,668.00 | 525,130.70 | 350,087.14 | 2,975,740.16 |
| SEPT-OCT 2014 | 38,919,158.00 | 34,594,808.00 | 589,684.23 | 393,122.82 | 3,341,542.95 |
| NOV-DEC 2014 | 43,659,000.00 | 38,808,000.00 | 661,500.00 | 441,000.00 | 3,748,500.00 |
| JAN-FEB 2015 | 43,668,000.00 | 38,816,000.00 | 661,636.36 | 441,090.91 | 3,749,272.73 |
| MAR-APR 2015 | 43,744,500.00 | 38,88,000.00 | 662,795.45 | 441,863.54 | 3,755,841.91 |
| MAY-JUNE 2015 | 42,043,500.00 | 37,372,000.00 | 637,022.73 | 424,681.82 | 3,609,795.45 |
| JULY-AUG 2015 | 43,578,000.00 | 38,736,000.00 | 660,272.73 | 440,181.82 | 3,741,545.45 |
| SEPT-OCT 2015 | 40,045,500.00 | 35,596,000.00 | 606,750.00 | 404,500.00 | 3,438,250.00 |
| NOV-DEC 2015 | 39,528,000.00 | 35,136,000.00 | 598,909.09 | 399,272.73 | 3,393,818.18 |
| JAN-FEB 2016 | 45,171,00.00 | 40,152,000.00 | 684,409.09 | 456,272.73 | 3,878,318.18 |
| MARCH-APRIL 2016 | 44,703,000.00 | 39,736,000.00 | 667,318.18 | 451,545.45 | 3,838,136.36 |
| MAY-JUNE 2016 | 44,059,500.00 | 39,164,000.00 | 667,568.18 | 445,045.45 | 3,782,886.36 |
| JULY-AGOST 2016 | 43,920,000.00 | 39,040,000.00 | 665,454.55 | 443,636.36 | 3,770,909.09 |
| SEPT-OCT 2016 | 46,786,500.00 | 41,588,000.00 | 708,886.36 | 472,590.91 | 4,017,022.73 |
| NOV-DEC 2017 | 46,989,000.00 | 41,768,000.00 | 711,954.55 | 474,636.36 | 4,034,409.09 |

| | | | | | |
|-------------------|-----------------------|-----------------------|----------------------|---------------------|----------------------|
| JAN-FEB 2017 | 43,609,500.00 | 38,764,000.00 | 660,750.00 | 440,500.00 | 3,744,250.00 |
| MAR-APRIL 2017 | 44,397,000.01 | 39,464,000.00 | 672,681.82 | 448,454.55 | 3,811,863.64 |
| JUMLA | 806,591,785.59 | 716,970,476.00 | 12,221,087.75 | 8,147,391.78 | 69,252,830.05 |

MIRADI YA AJIRA YA MUDA (PUBLIC WORKS PROGRAM-PWP)

Manispaa ya Mtwara Mikindani kwa mwaka 2014/2015 na mwaka 2016/17 imetekeleza miradi ya ajira ya muda kwa mitaa 35 ikijumuisha miradi mbalimbali ya ujenzi na mazingira, ambayo iliwezesha walengwa 1290 kujiongezea kipato kwa kushiriki katika miradi hiyo ikiharimu Jumla ya **Tshs.156,963,400.00** kwa mwaka 2014/15 na **Tsh 177,606,000.00** kwa mwaka 2016/17 kwa mitaa yote kwa muda wa miezi 4 ambapo walengwa walistahili kufanya kazi kwa muda wa siku 60 sawa na siku 15 kila mwezi kulingana na taratibu na kanuni za Mpango.

2.2.1 MADHUMUNI YA MIRADI YA MUDA

- Kujenga miundo mbinu ya Jamii
- kudhibiti na kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya Nchi
- Kuongeza kipato cha kaya hasa kipindi cha hari
- kuhamasisha walengwa kujenga utamaduni wa kufanya kazi na kuongeza ujuzi kupitia ushiriki wao kwenye miradi.

2.3.0 MIRADI YA UJENZI WA MIUNDO MBINU YA JAMII

Manispaa ya Mtwara- Mikindani kupitia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya jamii imetekeleza mradi wa kujenga Nyumba ya Mganga katika Mtaa wa Rwelu (Zahanati ya Lwelu) ambayo iliharimu kiasi cha **Tsh.66,180,500.00**. Utekelezaji wa miradi hii katika maeneo Mengine ya Mpango utategemea mipango na mikakati ya utekelezaji wa TASAF Makao Makuu ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa fedha.

2.3.1 MADHUMUNI YA MIRADI YA MIUNDO MBINU

- Kujenga utamaduni wa jamii kushiriki katika miradi ya maendeleo kwa kuchangia fedha au nguvu kazi.
- Kuboresha ,kuirimarisha na kuondoa upungufu wa miundo mbinu ya Jamii katika eneo husika

- Kuandaa mazingira bora ya Jamii kupata hudumu za Afya,Elimu na maji.

2.4 MIRADI YA KUWEKA AKIBA NA KUWEKEZA

Manispaa ya Mtwara Mikindani ina jumla ya ya vikundi 76 vya kuweka akiba na kuwekeza kwa walengwa wote waliopo katika mpango ambapo kila kikundi kina walengwa 10 hadi 15 na na mpaka sasa kuna Vikundi 33 vimeanza kuweka Akiba na kuwekeza katika miradi midogo midogo ambayo kwa sasa wameweza kukusanya **TSH 9,124,000.00**.

- Lengo kuu ni la walengwa kujiunga vikundi vya kuweka Akiba ni kukuza utamaduni wa kujiwekea akiba kwa kaya maskini ili kuwawezesha kukabiliana na dharura na mahitaji ya msingi

2.4.1 MALENGO KUHAMASISHA KAYA KUWEKA AKIBA NA KUWEKEZA

- Kutoa fursa kwa kaya maskini kufikia na kupata huduma za kifedha kutoka kwenye akiba waliyojiwekea na kuwekeza kwenye miradi ya kiuchumi
- Kusaidia kuanzishwa kwa mtandao utakaowawezesha kupashana habari zitakazowasaidia kutekeleza shughuli zao ipasavyo.
- Kuwezesha vikundi/vyama vya kuweka akiba na kuweza kuunganishwa na taasisi za fedha
- Kutoa fursa kwa kaya maskini kama kikundi,mmojammoja kufikia na kupata huduma za kifedha kutoka kwenye akiba za vikundi, vyama na taasisi mbalimbali za fedha.

3.0 UKELEZAJI WA SHUGHULI CHA MRADI CHA TASAF

Mradi unatekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na idara zote katika halmashauri kwa kutegemea aina miradi iliyoibuliwa,kusanifiwa na inayotekezwa(Uratibu kisékta), vile vile kwa kuzingatia umuhimu wa TEHAMA Mfumo wa compyuta ndio hutumika kuingiza taarifa za kaya,kuandaa mchakato wote wa malipo na nyaraka zote zinahitajika wakati wa zoezi la malipo, kushughulikia malalamiko na madai ya walengwa pale yanapojitokeza.

3.1 MAFANIKIO YALIYOFIKIWA HALMASHAURI KUPITIA TASAF

- Kuboreka kwa lishe kutoka lishe duni kwenda lishe bora na idadi ya milo toka mmoja hadi mitatu kwa Kaya
- Kuongezeka kwa mahudhurio ya wanafunzi wa shule za msingi na Sekondari wanaotimiza masharti
- Kuanzishwa kwa miradi mbalimbali yenye kuongeza kipato
- Kuundwa kwa vikundi vya kuweka na kukopa 76 kutoka katika Kaya maskini

- Kaya Maskini kuchangia mfuko wa Afya ya Jamii (TIKA),CHF
- Kuboresha miundo mbinu kupitia miradi ya nguvu kazi na Ajira za muda